

---

Ikiwa una wasiwasi wowote kwamba binti yako anapanga kusafiri Syria (au eneo lolote lenye mzozo) unastahili kuwasiliana na polisi wa eneo lako au upige simu 101. Wakati wa dharura Piga simu kwa 999. Wataongea na wewe faraghani kuhusu wasiwasi wako na watafanya kazi pamoja na wewe na mawakala wataalamu ili kukuunga mkono na kukusaidia wewe na familia yako. Hii inahusu kuzuia misiba na sio kuhusu kuwashtaki vijana kwa uhalifu.

Ikiwa huhisi sawa kuongea na polisi moja kwa moja kuhusu hoja zako, kuna watu wengine ambao wamefunzwa na wanaweza kutoa msaada na usaidizi halisi kwako na familia yako. Hawa ni pamoja na waatalamu wa huduma ya afya, wafanya kazi wa kijamii, walimu na utawala wa eneo lako. Jambo la maana sana ni kwamba utafute msaada mapema kutoka kwa mtu.

Kwa maelezo sahihi kuhusu hali ya sasa nchini Syria tembelea

[www.gov.uk/foreign-travel-advice/syria](http://www.gov.uk/foreign-travel-advice/syria)

## Polisi na Washirika wa Uingereza Kufanya kazi pamoja na akina mama ili kuzuia misiba

---

---

Kampeni ya Kuzuia Misiba (Prevent Tragedies), kwa ushirikiano na Polisi wa Uingereza na washirika wake.  
[www.preventtragedies.co.uk](http://www.preventtragedies.co.uk)



# Syria - ukweli

Baadhi ya mabinti wetu wametekwa nyara, kushawishiwa na kulamizishwa kusafiri Syria.

Syria ni mahali pabaya sana. Wanawake na wasichana wanaosafiri Syria wana uwezekano wa kushuhudia ukatili mbaya sana, wanaweza kuwa wahasiriwa wa ukatili, au katika hali nyingine, wanaweza kuhusishwa katika kutenda vitendo vya ukatili. Hata kama hawatajipata katika hatari ya moja kwa moja, uhuru na nafasi zinazochukuliwa kimzaha katika nchi hii sio hivyo kwa wanawake wa Syria. Huenda wakajipata peke yao na wametengwa, wanaishi chini ya utawala unaonyanyasa, na mara kwa mara hawawezi kutoka nyumbani mwao, wala kurejea katika nchi zao za nyumbani. Familia zao zitaachwa zimehuzunika na bila chaguo lolote la kuhakikisha kurejea kwa wapendwa wao.

Picha na propaganda zinazovutia zinazokuzwa mtandaoni, pamoja na maneno ya kupotosha ya wale wanaotafuta kuwageuza vijana wadogo wanaoweza kuathiriwa na kuvutiwa katika jamii zetu, wanawahimiza baadhi ya wanawake na wasichana kusafiri Syria. Katika hali zingine mvuto huo unaweza kuwa 'mvutio' wa kuolewa na mpiganaji, au wanaweza kuchanganikiwa kuhusu njia ya kupatanisha dini yao na maisha ya kisasa, na kuhisi kulazimika kufuata majukumu yao ya kidini kwa kujiunga na wale wako Syria.

Lakini kama tujavyo, ukweli wa maisha nchini Syria hadi sasa sio kama picha tunayoonyeshwa.

Hatusikii kuhusu wanawake na wasichana wale ambao wanataka sana kurejelea familia zao. Sauti zao zimepotea.

Hakuna mzazi angetaka kuona mtoto wake akiwa hatarini, akitumiwa vibaya au katika hali ambayo anaweza kufariki. Ni huzuni kwamba, hadithi za familia ambazo zimepitia matokeo mbaya ya wanawake na wasichana ambao wamesafiri Syria na kutorejea zimekuwa za kawaida sana.

# Je, familia zinaweza kufanya nini?

Kuna hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa mapema ili kuwalinda vijana wetu kabla ya kuanza kuzingatia kusafiri Syria.

Akina mama ndio mara kwa mara huwa wale katika familia ambao wana uwezekano mkubwa wa kuona ishara na kugundua mabadiliko katika tabia ya watoto wao. Wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuwashawishi watoto wao wasisafiri.

Akina mama wanaweza kuwalinda wapendwa wao kabla ya mambo kuharibika kwa kuchukua hatua kama vile kufuatilia yale mabinti wao wanatafuta mtandaoni, kuhimiza mazungumzo wazi kuhusu masuala ambayo yanawahusu.

---

**Kalloom Bashir kutoka INSPIRE alisema:** *“Baada ya kuona huzuni inayokabili familia ambazo wapendwa wao wamesafiri Syria, ningependa kushauri familia wawaweke watoto wao karibu - wawakumbushe mara kwa mara kuwa wanapendwa, kuwa ni sehemu ya mtandao wa familia dhabiti na kwamba wanaweza kuongea na wewe kuhusu kitu chochote ambacho kinawasumbua.”*

Ikiwa una wasiwasi kwamba binti yako huenda tayari anafikiria kuhusu kusafiri Syria, mara kwa mara huwa kuna ishara za kuangalia, ambazo zinaweza kujumuisha:

- Kuomba kuwa na pasipoti na hati zingine za utambulisho kama vile vyeti vya kuzaliwa na leseni ya kuendesha gari - sio yake tu bali za washirika wengine wa kike wa familia.
- Anajiandaa kusema kwaheri.
- Ghafila anaanza kutafuta mavazi mapya au kuweka pesa kwenye akiba.
- Huenda binti yako akaacha kutangamana na marafiki wake wa kawaida, au awe na marafiki wapya ambao hujawahi kuwaona awali ambao wanaonekana kumshawishi vibaya.
- Huenda akaanza kuonyesha dhana, kwa kuongea au kwenye vyombo vya kijamii, ambazo zinaegemea dhana au hatua za watu wenye misimamo mikali, au kuanza kuvutiwa na siasa au sera za kigeni ambapo awali hakuwa akivutiwa.